

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA PILI**

**KIKAO CHA NANE**

**11 FEBRUARI, 2021**



# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA PILI

KIKAO CHA NANE – TAREHE 11 FEBRUARI, 2021

### I. DUA:

### II. KIAPO CHA UAMINIFU:

1. Mhe. Ameir Abdalla Ameir
2. Mhe. Bakar Hamad Bakar
3. Mhe. Bahati Khamis Kombo
4. Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis
5. Mhe. Suleiman Haroub Suleiman

### III. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:

### IV. MASWALI YA KAWAIDA:

#### OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

#### 103. MHESHIMIWA MAIMUNA SALUM MTANDA (NEWALA VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Halmashauri ya Wilaya ya Newala ina Kata 22 na Vijiji 107 lakini ina

Vituo vya Afya vitatu tu kati ya 22 vinavyohitajika:-

Je, Serikali haioni haja ya kujenga Vituo vipya vya Afya katika Halmashauri ya Newala ili kuboresha huduma za afya kwa Wananchi.

**104. MHESHIMIWA GRACE VICTOR TENDEGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Akina Mama wajawazito wamekuwa wakitozwa fedha kuanzia Shilingi 50,000 hadi 70,000 wasipojifungulia katika Vituo vya Afya hasa katika Jimbo la Kalenga; huku Vituo hivyo vikiwa mbali na maeneo wanayoishi: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kujenga maeneo ya kusubiri kujifungua katika Vituo vya Afya.

**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:**

**105. MHESHIMIWA ABUBAKAR DAMIAN ASENGA (KILOMBERO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Fedha na Mipango:-

Je, ni lini Serikali itaongeza uwekezaji wa Kiwanda cha Sukari Kilombero ili kunusuru

Miwa ambayo haijavunwa kwa zaidi ya mwaka mmoja sasa.

## **WIZARA YA MADINI:**

### **106. MHESHIMIWA ORAN MANASE NJEZA (MBEYA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

Je, ni lini uzalishaji wa madini ya *Niobium* utaanza katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

### **107. MHESHIMIWA DKT. PIUS STEPHEN CHAYA (MANYONI MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya utafiti ili kubaini uwepo wa aina mbalimbali za madini katika Jimbo la Manyoni Mashariki hususan Kata za Sasilo, Makuru, Kintinku na Solya.

## **WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

### **108. MHESHIMIWA MWANAISHA NG'ANZI ULENGE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:- Miradi mikubwa ya

ujenzi nchini inafanywa na Kampuni kutoka Bara la Asia wakati Wahandisi nchini wanasoma Uhandisi kwa Mitaala ya Uingereza na Marekani:-

(a) Je, Serikali haioni haja ya kuongeza Mitaala ya Asia katika Mitaala ya Vyuo vya Uhandisi ili Wahandisi wetu wapate utaalam katika miradi ya ujenzi;

(b) Je, suala la kubadilishana weledi limepewa kipaumbele gani katika miradi inayoendelea kujengwa hapa nchini.

**109. MHESHIMIWA BONIPHACE MWITA GETERE (BUNDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kukamilisha dhana ya elimu bure kwa kutoa elimu bure kuanzia Shule ya Msingi hadi Kidato cha Tano na cha Sita.

**WIZARA YA MAJI:**

**110. MHESHIMIWA ISSA ALLY MCHUNGAHELA (LULINDI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-  
Mradi wa maji wa Chipingo uliopo katika Jimbo

la Lulindi ambao umegharimu Shilingi Bilioni 3.9 ni wa muda mrefu tangu mwaka 2013 lakini umekuwa hauna tija kwa kuwa hautoi maji; mabomba kupasuka mara kwa mara na mpaka sasa bado haujakabidhiwa kwa Serikali:-

Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya mradi huo.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**111. MHESHIMIWA AGNESTA LAMBERT KAIZA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni nini kauli ya Serikali kuhusu ucheleweshaji wa kupandisha vyeo kwa Askari wa Jeshi la Polisi katika ngazi ya Wakaguzi Wasaidizi na kwa Wakaguzi.

**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

**112. MHESHIMIWA ATUPELE FREDY MWAKIBETE (BUSOKELO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini ujenzi wa Daraja la Mto Mbaka linalounganisha Jimbo la Busokelo na Rungwe utakamilika.

**113. MHESHIMIWA GODWIN EMMANUEL KUNAMBI (MLIMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:- Serikali ina mpango wa kuunganisha Mikoa yote kwa mtandao wa barabara za kiwango cha lami, ikiwemo barabara yenye urefu wa Km 223 inayounganisha Mikoa ya Njombe na Morogoro kupitia Mlimba ambayo pia ipo katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM):-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara hiyo.

**V. HOJA ZA SERIKALI:**

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Kwamba, Bunge sasa lipokee, kujadili na kushauri kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26) na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2021/22 pamoja na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2021/22.

*(Majadiliano yanaendelea)*

**DODOMA  
11 FEBRUARI, 2021**

**S. KAGAIGAI  
KATIBU WA BUNGE**